

TAARIFA YA MUHIMU YA WILAYA YA CHEMBA

1.1 UTANGULIZI

Wilaya ya Chemba ilianzishwa mwezi march 2013 baada ya kugawanya wilaya ya Kondo. Aidha halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilianzishwa Kwa mujibu wa sheria ya serkali za Mitaa na. 287 ya Mwaka 2002, kifungu na. 8 na 9. Mipaka yake ni ile ya iliyokuwa ya jimbo la uchaguzi la Kondo kusini. Kwa upande wa Mashariki imepakana na Wilaya ya Kiteto, Kusini imepakana na Wilaya ya bahi na Chamwino, Magharibi imepakana na Wilaya ya Ikungi na Kaskazini imepakana na Wilaya ya Kondo. Wakazi wa Wilaya ya Chemba ni Makabila ya Warangi, Wagogo, Waburunge, Wasandawi na Wanguu. Aidha makabila wahamiaji ya Wamasai, wabarbaig ni wakazi pia wa Wilaya ya Chemba.

Mazao Makuu ya Chakula ni Mahindi, Alizeti, Mbaazi, Mpunga na mtama. Mazao ya biashara ni Alizeti, Karanga, Ufuta na Dengu

(a) UTAWALA.

Wilaya ya Chemba ina jumla ya Tarafa **4**, Kata **20**, Vijiji **95** na Vitongoji **530**

(b) IDADI YA WATU.

Kwa mujibu wa sensa ya watu ya mwaka 2012 wilaya ilikadiriwa kuwa na watu **235,711** Wakiwemo wanaume **117,585** na wanawake **118,126** ikiwa ni ongezeko la asilimia **1.7** kwa mwaka

(d) HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO YA WILAYA.

- Mapato ya wakazi wa wilaya ya Chemba yanatokana na Kilimo, ufugaji, urinaji asali, Pato la Wilaya Aidha pato la mtu kwa mwaka Tsh. **1,560,000**

1.2 MPANGO NA BAJETI YA WILAYA.

Mwaka wa fedha 2013/2014 Wilaya iliidhinishiwa jumla ya Tshs **21,706,921,235.00** Kati ya hizo shs **8,015,147,130.00** ni za miradi ya maendeleo na shs **13,711,724,105.00** Ni matumizi ya kawaida. Mapokezi ya fedha yalikuwa ni shs. Sawa na asilimia..... Katika bajeti ya Mwaka

2014/15 Wilaya imeidhinishiwa jumla ya shs.....Kati ya hizo shs. Nia miradi ya maendeleo, shs..... Matumizi mengineyo.....na shs..... mishahara

1.3

1.4 **MAKUSANYO YA NDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**

Kwa mwaka wa fedha 2013/14 Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilikisia kukusanya jumla Tshs **925,000,000** Hadi kufikia mwezi Juni 2014, Halmashauri imekusanya jumla ya Tshs ambayo ni sawa na asilimia ... ya malengo. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 Halmashauri imekadiria kukusanya jumla ya Tshs **1,427,969,000** sawa na ongezeko la asilimia **31** ukilinganisha na makisio ya mwaka wa fedha wa 2013/14.

1.5 **WATUMISHI WA HALMASHAURI.**

Halmashauri ina jumla ya watumishi **1531** kati yao watumishi **104** wako makao makuu ya wilaya na **94** ngazi ya kata na vijiji. Watumishi hao wamegawanyika katika sekta elimu **1202**, Afya **106**, kilimo na mifugo **83**, maendeleo ya jamii **8**, Utawala **115**, mipango **5**, Maliasili **6**, Ardhi na mipangomiji **3**, Maji **3**.

1.4 **KANDA ZA IKOLOGIA (ECOLOGICAL ZONES):**

Wilaya ya Chemba inapatikana kati ya Longitude Mashariki mwa Greenwich na Latitude Kusini mwa Ikweta; Wilaya ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba **7,653**

1.5 **ENEO LA KILIMO.**

Chemba ina eneo lipatalo km² **7,653** Eneo linalofaa kwa kilimo ni Ha **925,000** Eneo linalolimwa ni Ha **222,184** ambalo ni asilimia 24 Eneo la Malisho ni km² **957**, eneo la vichaka na misitu Ha **702,816** na Eneo la Hifadhi ya wanyama pori Swagaswaga ni Ha **403,216**

1.7 **KANDA ZA MVUA.**

Wilaya hupata mvua ya wastani wa 740mm kwa mwaka. Msimu wa mvua huanza mwezi Desemba na kuishia mwezi mei Kiwango cha juu cha Joto ni **31°C** na kiwango cha chini cha joto ni **26°C**. Kuna kanda 2 za mvua :-

a) Kanda ya mvua nyingi wastani wa mm **750** Hii inajumuisha Tarafa za Kwamtoro

b) Kanda ya mvua chache wastani wa mm **600**

Hii inajumuisha Tarafa za Goima

2.0 SHUGHULI ZA KIUCHUMI KISEKTA

2.1 SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA.

Wilaya ya Chemba ina ukubwa wa kilometa za mraba **7,653** . Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta **925,000** ambalo linalimwa kwa sasa ni hekta **152,495** ikiwa ni 16% tu ya eneo lote linalofaa kwa Kilimo.

Hali ya kilimo bado ni duni kutokana na wakulima wengi kuwa na mwitikio mdogo wa kutumia pembejeo bora za kilimo hususani mbegu na Mbolea. Aidha wakulima wengi hawazingatii kanuni bora za kilimo kama vile Kutopanda kwa nafasi zinazopendekezwa, kutotumia madawa ya kuzuia visumbufu vya mazao. Ili kukabiliana na tatizo hili wilaya inaendelea kusisitiza uanzishaji wa mashamba darasa

2.2 HALI YA CHAKULA

Hali ya chakula kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwa sasa ni ya kuridhisha kwani wakulima wameshavuna mazao mbalimbali mashambani kama vile mahindi, maharage (mimea jamii ya kunde), maboga, alizeti, uwele, karanga, mpunga n.k.

Pamoja na hivyo, mahitaji ya chakula kwa mwaka 2013/2014 ni tani **52,498** kwa mazao ya nafaka. Lengo la uzalishaji wa mazao ya chakula na hasa nafaka lilikuwa ni tani **157,974** na mavuno yaliyopatikana ni tani Sababu ya kutofikia malengo tuliyoweka ilitokana na athari ya ukame uliojitokeza pamoja na mtawanyiko wa mvua kutokuwa mzuri. Hali hii inaweza kusababisha upungufu wa chakula kwa baadhi ya maeneo ya Wilaya. Ofisi inaendelea kuelimisha wakulima kutunza chakula wanachovuna pamoja na kulima viazi vitamu (Lishe) katika maeneo yao ili kuweza kuepuka upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza.

Jedwali Na.1 utekelezaji wa malengo ya kilimo kwa mwaka 2012/13 na mwaka 2013/14.

2012/13					2013/14			
	Lengo		Utekelezaji		Lengo		Utekelezaji	
Zao	Ha	Tani	Ha	Tani	Ha	Tani	Ha	Tani
Nafaka								
Mtama	29,833	35,800	22,375	20,137	32,560	39,072	24,120	
Uwele	31,964	38,357	23,973	21,575	34,600	41,520	25,270	

Mahindi	34,095	68,191	25,571	38,357	35,236	70,472	28,808	
Mpunga	426	426	6,392	14,383	598	598	438	
Ulezi	7,245	5,796	5,433	3,260	7,890	6,312	6656	
Jumla	103563	148570	83744	97712	110884	157974	85292	
Mizizi								
Mihogo	8,524	25,572	6,392	14,383	9,490	28,470	8,652	
Viazi vitamu	2,131	6,393	1,598	3,596	3,470	10410		
Jumla	10655	31965	7990	17979	12960	38880		
Mikunde								
Maharag e	2,983	1,193	2237	671	31,400	12,560	2290	
Kunde	2,557	1,023	1,917	575	3,245	1,298	2,100	
Mbaazi	21,310	17,048	15,982	9,589	24,652	19721.6	18,210	
Njugu mawe	1,705	682	1,278	383	19,230	7,692	1,6780	
Jumla	28555	19946	21414	11218	78527	41271.6	39380	
Mafuta								
Karanga	12,786	8,950	9,589	5,034	13,894	9725.8	10,203	
Alizeti	29,833	35,800	22,375	20,137	33,168	39,801.6	24,128	
Ufuta	7,671	4,603	5,753	2,589	8,990	5,394	7,970	
Koroshu	34	102	25	56	35	105	25	
Jumla	50324	49455	37742	27816	56087	55026.4	42326	

2.5: Changamoto za utekelezaji wa malengo

- Ndege waharibifu (kwelea kwelea), jambo linalosababisha uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame kama uwele na mtama kupungua.
- Uharibifu wa Mazingira
- Magonjwa ya mimea hususani ugonjwa wa ukungu kwenye zao la Alizeti
- Migogoro ya Ardhi kwenye baadhi ya maeneo

2.6 Mikakati ya kupunguza changamoto hizo

- Kuimarisha vikundi vya wakulima ili waweze kuagiza zana za kilimo na pia kuwa nguvu katika soko.

- Kuboresha huduma ya ugani kwa kuwapa maafisa ugani uwezo wa kuwafikia wakulima waliopo vijijini.
- Kuanzisha mashamba ya mfano na mashamba darasa katika kila kijiji.
- Kusaidia kuanzishwa kwa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo kwa wakulima na wafugaji.
- Ujenzi wa maghala ambayo yatasaidia kuhifadhi mazao ya wakulima mpaka wakati utakaofaa kwa mauzo.
- Kuendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wakulima juu ya mazao haya ili kuwa na usalama wa chakula katika kaya.

2.7 HUDUMA ZA UGANI

Huduma za ugani ni muhimu kwa uzalishaji wenye tija. Wilaya ya Chemba ina mahitaji makubwa ya watumishi wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika na hasa katika ngazi za Kata na Vijiji. Watumishi wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika walioko ngazi ya kata na vijiji wako 15 na wa makao makuu wako 6. Upungufu wa watumishi wa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika ni 108

Jedwali na. 1 :-Vitendea kazi

S/N		Mahitaji	Zilizopo	Upungufu
1	Nyumba	115	9	106
2	Pikipiki	120	15	105
3	Extension Kit	115	5	110
4	Gari	2	0	2

2.7.1 Mbinu za kuziba pengo la Wataalam Mashamba darasa (FFS) ya kilimo

Wilaya inatumia mashamba darasa kama mbinu mojawapo ya kuziba pengo la wataalam. Mashamba darasa hutumika kuwaelimisha wakulima mbinu mbalimbali za ukulima bora.

Wilaya imewaagiza wataalamu wa ngazi ya kata na vijiji kuwa na mashamba ya mifano au darasa kwa ajili ya wakulima kujifunza. Kwa mwaka huu 2013/2014 kulikuwa na mashamba darasa ... ya zao la mtama, mashamba darasa ya mahindi na mashamba darasa ya alizeti yako

Pia kuna mashamba ya majaribio (demo plots) katika vijiji vya Mondo na Paranga kwa ajili ya Kilimo hifadhi.

2.9 MAHITAJI YA PEMBEJEO:

Mahitaji ya Pembejeo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ni makubwa kwani sehemu kubwa ya udongo wake ni kichanga na sehemu zingine rutuba imepungua kwa kiwango kikubwa kwani hulimwa kila mwaka(bila kupumzisha shamba).

Hali hii husababisha njaa kwa wakazi wa Wilaya hii mara kwa mara na kwa mantiki hii uhitaji wa pembejeo za Kilimo ni mkubwa.

Mahitaji ya samadi kwa Wilaya nzima yanakadiriwa kuwa tani milioni 2,221,840. Upatikanaji wake ni tani.....na matumizi yake kwa sasa ni tani laki mbili tu kwa mwaka kutokana na ugumu wa upatikanaji wake. (Wastani wa tani 10 kwa hekta). . Wilaya ya Chemba kupitia sheria ndogo inayohusu usambazaji wa samadi kutoka kwenye mazizi kwenda mashambani (Suji kumgunda) imehamasisha wakulima kusambaza mbolea mashambani na mpaka sasa utekelezaji wake ni asilimia 61.14.

Mahitaji ya mbolea za viwandani kwa mwaka yanakadiriwa kuwa ni tani 62211.5 ambapo matumizi ya sasa kwa mwaka yanakadiriwa kuwa tani 2,200

Aidha katika msimu wa kilimo 2013/14 Wilaya haipo kwenye mpango wa pembejeo za ruzuku kwa mfumo wa vocha, hivyo wakulima wameshauriwa kutumia mbolea ya samadi kwa wingi pamoja na kununua pembejeo zingine kutoka kwa mawakala.

2.10 UPATIKANAJI WA ZANA:

Zana za Kilimo zinapatikana katika maduka, masoko,minada,makampuni,mashirika na taasisi mbalimbali kama vile **SUMA JKT,NAM** n.k. Zana zinazopatikana katika maeneo tajwa hapo juu ni Jembe la mikono,Jembe la kukokotwa na Wanyama,Power Tiller,Tractor n.k.

Kwa hiyo wakulima wanashauriwa kununua zana hizo katika maeneo hayo ili kuweza kuendesha shughuli za Kilimo kitaalamu. Katika msimu uliopita wakulima ...walikopeshwa jumla ya power tiller 5.

Jedwali na.2: Matumizi ya Zana za Kilimo

Aina ya zana	Binafsi	Kikundi
Jembe la kutifua (Sub-soiler)	137	0
Jembe la kupalilia (Weeder)	Mengi	-
Jembe la kukatua (Ripper)	6708	8
Jembe la matuta (Ridger)	-	0

Mkokoteni (Cart)	9	4
Trekta (Tractor)	150	3
Trekta la mkono (Power tiller)	16	65
Mashine za kusindika Alizeti	41	2

2.11 KILIMO CHA UMWAGILIAJI

S/n	Jina la Mradi	Mahali ulipo (Kijiji/Vijiji)	Eneo linalofaa kwa umwagiliaji (Ha)	Eneo linalomwagiliwa kwa sasa (Ha)
1.	Jogolo	Jogolo	1000	5
2.	Kidoka	Kidoka	1000	5
4.	Kelema Balai	Kelema Balai	100	15
5	Lahoda	Lahoda	10	1
6	Takwa	Takwa	30	1
7	Paranga	Paranga	1000	200

WADAU WANAOTOA HUDUMA ZA KILIMO.

Taasisi zinazotoa huduma mbalimbali hapa wilayani ni pamoja na Agriculture Seed Agent, Three Sisters CO.Ltd, INADES, ADP, ICCRISAT, Africare, World Food Programme

3.0 SEKTA YA MIFUGO

Wilaya ya Chemba inakadiriwa kuwa na jumla ya mifugo kama ifuatavyo ng'ombe 278,666 wa asili na 131 wa kisasa, mbuzi wa asili ni 184,569 na wa kisasa 283, kondoo 86,667, nguruwe 600, kuku 352,000, bata 120,000, punda 12,933, mbwa 3,081, paka 600 na sungura 5,400.

Hali ya ufugaji katika wilaya ya Chemba ni ile ya kuhama hama kwa ajili ya kutafuta malisho na maji.

Mifugo ifugwayo ni ile ya asili kwa asilimia kubwa japo wapo wafugaji wachache wanaojihusisha na ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Njia inayotumika katika ufugaji ni ile kupeleka mifugo machungani na jioni kuirudisha kwenye maboma/mazizi (free range grazing system). Asilimia kubwa ya wananchi wa Wilaya ya Chemba ni wakulima-wafugaji (agro-pastoralist) ambao licha ya kufuga tu pia hujihusisha pia na shughuli za kilimo.

mpango wa matumizi bora ya ardhi umefanyika mahsusi kwa ajili ya kupata eneo la malisho Katika vijiji 4 vya Pangalua, Lahoda, Handa na Kisande ambalo litamilikiwa na wafugaji wenyewe na kwasasa zoezi lipo

katika hatua za mwisho za kuandaa hati miliki. Jumla ya ha 8,892 zimepimwa kwa ajili ya malisho ya mifugo ya pamoja katika vijiji vya Handa, Lahoda na Kisande (LAHAKI). Aidha jumla ya ha 1,247.37 zimetengwa katika kijiji cha Pangalua.

3.1 MARADHI YA MIFUGO.

Kuna maradhi mbalimbali yanayoathiri Mifugo. Maradhi hayo ni yanayotokana na kupe kama ndigana kali, ndigana baridi, mkojo mwekundu nk. Hata hivyo magonjwa mengine yanayosumbua mifugo ni minyoo, chambavu, ugonjwa wa miguu na midomo (FMD), ugonjwa wa mapafu (CCPP - mbuzi) ambayo hutokea kwa kipindi.

3.2 HUDUMA YA MIFUGO.

Huduma zitolewazo ni pamoja na uogeshaji, unyunyiziaji, tiba, chanjo, kuhasi, ushauri, ukaguzi wa nyama, usimamizi wa minada na utoaji wa vibali kwa mifugo inayosafirishwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uendelezaji maeneo ya malisho, uhamilishaji (Artificial Insemination) na huduma za ugani.

Jedwali na.4 watumishi sekta ya mifugo:

KIWANGO CHA ELIMU	IDADI		
	Me	Ke	Jumla
Uzamili	-	-	-
Shahada	4	3	7
Stashahada	15	4	19
Astashahada	-	-	-
Kozi mwaka mmoja	-	-	-
JUMLA	19	7	26

Jedwali Na. 5 miundo mbinu ya mifugo iliyopo:

Miundombinu	Idadi	Mazima	Yanayofan ya kazi	Mazima yasiyofanya kazi	Yanayokarabati wa	Yanayo jengwa	Mabovu
Majosho	19	10	6	4	-	-	9
Malambo	25	18	18	-	3	1	4
Minada	18	18	18	-	-	-	-
Mabanda ya Ngozi	11	-	-	-	-	-	11

Jedwali Na. 6:- MAUZO YA MAZAO YA MIFUGO

Zao	Mwaka 2013/2014	Mwaka 2014/2015	Mwaka 2015/2016
-----	-----------------	-----------------	-----------------

	Idadi	Thamani (Tshs)	Idadi	Thamani (Tshs)	Idadi	Thamani (Tshs)
Maziwa	351,840	175,920,000				
Kuku	81,920	309,600,000				
Ng'ombe	19,844	4,961,000,000				
Mbuzi	8,676	347,040,000				
Kondoo	1,476	51,660,000				

3.4 CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MIFUGO

- Upungufu wa watumishi wenye fani ya mifugo.
- Ukosefu wa usafiri kama pikipiki na gari kwaajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za ufugaji.
- Uelewa mdogo wa jamii juu ya uchangiaji wa huduma za mifugo.
- Idadi ndogo ya wataalam waliopitia mafunzo ya upandishaji kwa njia ya chupa (AI).
- Ukosefu wa vifaa vya uhimilishaji (AI) pamoja na vifaa vingine vya huduma za mifugo kama friji kwaajili ya uhifadhi wa chanjo n.k

3.5 MIKAKATI YA KIWILAYA KATIKA SEKTA YA MIFUGO

- Kuendelea kuwaelimisha na kuwashauri wafugaji kupitia mashamba darasa juu ya Ufugaji bora.
- Kuendelea kuhamasisha wafugaji juu ya upandishaji kwa njia ya chupa - uhamilishaji (Artificial Insemination)
- Kuweka bajeti na kuendelea kujenga na kukarabati na kujenga majosho, malambo kwaajili ya mifugo ili kunusuru vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa ya kupe ambayo ni tatizo kubwa wilayani.
- Kupeleka na kuhamasisha wataalam wa mifugo kwenda kusoma mafunzo ya muda mfupi juu ya upandishaji (Artificial Insemination)
- Kuendesha mikutano ya kuhamasisha juu ya kanuni za Ufugaji bora.

4.0 USHIRIKA

Wilaya ina jumla ya vyama vya msingi 11 vyenye jumla ya wanachama 3224 kati yao ME 1911 na KE 1127 Vikundi na Taasisi 184. Vyama hivyo vina hisa zenye thamani ya Tshs 44,697,870, Akiba kiasi cha Tshs 127,184,903 na Amana kiasi cha Tshs 33,389,670/=

4.3 VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS)

Idadi ya vyama vya kuweka na kukopa ni vyenye jumla ya wanachama ...Mitaji katika vyama hivi ni jumla ya shs. Lengo la wilaya ni kuanzisha vyama ifikapo mwaka

4.4 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA USHIRIKA

- Kuwepo kwa sheria , kanuni na sera ya Ushirika inayowapa wanachama uwezo na muongozo wa kuendesha vyama vyao
- Viongozi wa vyama vya Ushirika wamekuwa wakichaguliwa na wanachama wake kwa kufuata maadili, uwezo, ujuzi na uaminifu kupitia mikutano mikuu ya mwaka.
- Ushirika umeanzishwa katika sekta mbali mbali za kiuchumi, mfano kilimo cha umwagiliaji, mazao, ufugaji nyuki, na wafanya biashara. Vyama vya Ushirika wa akiba na mikopo, Hivyo kuongeza kipato na kupunguza umaskini miongoni mwa wanachama wa Ushirika na jamii kwa ujumla.
- Mafunzo na ushauri wa kitaalam yametolewa kwa wajumbe wa bodi 35) na watendaji 8 yametolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kiuongozi na kiutendaji wa vyama vya Ushirika.

4.5 CHANGAMOTO ZINAZOVIKABILI VYAMA VYA USHIRIKA.

- Uelewa mdogo wa wananchi juu ya Ushirika.
- Ushindani wa kibiashara katika soko huru kwa vyama vya Ushirika.
- Bei ndogo ya mazao ya biashara.
- Kilimo cha kutegemea mvua kimekuwa tatizo kwa mikopo ya kilimo kutokana na uhaba wa mvua ndogo inayoyepekea wakulima wengi kukosa mavuno ya kutosha au kukosa kabisa na hivyo kushindwa kurejesha mikopo.
- Uaminifu mdogo wa viongozi wa vyama.
- Baadhi ya viongozi Kutokuwa wazi katika uendeshaji wa shughuli za vyama vya Ushirika.
- Mitaji midogo isiyoweza kukidhi mahitaji halisi ya wanachama.
- Mikopo mibaya (chechefu) inayosababishwa na baadhi ya wanachama wasio waaminifu hurudisha maendeleo na ukuaji wa vyama.
- Ukosefu wa fedha na vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji na kutoa mafunzo mbalimbali kwa wanachama.

4.6 MIKAKATI YA KUKABILI CHANGAMOTO:-

- Kutoa mafunzo kwa wanachamana viongozi wa vyama vya Ushirika juu ya mbinu mbalimbali za kumudu ushindani katika soko huru, kwa wakulima na kuongeza vipato vyao na vya vyama vyao kwa kulipa ushuru wa mazao, na kuhimiza wakulima/wanachama kulima mazao ya biashara ambayo watauzia vyama vyao mfano mpunga, ufuta na alizeti.
- Kuanzisha mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani ili kusaidia kutafuta bei nzuri kwa mazao ya wakulima.
- Kuimarisha SACCOS ziweze kutoa mikopo kwa wanachama wake ili waweze kujitafutia pembejeo.
- Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vyama vya ushirika wa Akiba na mikopo na kutoa ushauri wa kitaalamu wa viongozi na watendaji wa vyama.
- Kuhamasisha wananchi ili waweze kujiunga na vyama vya Ushirika.
- Kufanya ukaguzi wa hesabu na kumbukumbu za vyama za robo, nusu na mwaka.
- Kuziunganisha SACCOS na Taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo ili ziweze kukopa na kuongeza mitaji yao.

5.0 SEKTA YA MALIASILI NA MAZINGIRA.

5.1 MISITU

Misitu iliyohifadhiwa kisheria ina jumla ya eneo la Ha **6450.3** Misitu kwenye maeneo ya wazi ina jumla ya eneo la Ha **3062**. Changamoto kubwa tunayokabiliana nayo ni uharibifu wa misitu kutokana na kufungua maeneo mapya ya kilimo, uchomaji mkaa, uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Aidha kutokana na uhaba wa watumishi zoezi la kuthibiti uharibifu wa mazingira limekuwa na changamoto nyingi.

5.1.1 CHANGAMOTO

Ukosefu wa vitendea kazi kama usafiri, silaha pia matumizi ya tochi na honi elimu juu ya faida za wanyamapori, ukame unaowapelekea wanyama kutawanyika kwenye maeneo ya makazi hivyo kupelekea wanyamaporokuuawa. Upungufu wa watumishi wa kada hi ya hifadhi wanyamapori.

5.1.2 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

1. Kuomba vibali vya kuajiri watumishi wa kada husika

2. Kufanya dori za mara kwa mara katika katika maeneo yote ya wazi
3. Kuendelea kutoa elimu hifadhi ya misitu na faida zake
4. Kutunga sheria ndongo za vijiji ili kuzuia uharibifu wa mazingira unaopelekea maeneo mengi ya wanyamapori kuharibiwa kwa kufyekwa na kusababisha utawanyikaji wa wanyamapori katika makazi.

5.2 UFUGAJI NYUKI WILAYANI

Ufugaji wa nyuki Wilayani unafanyika ndani ya misitu ya hifadhi na kwenye maeneo ya vijiji vilivyo jirani na misitu mikubwa

Jedwali Na. Uzalishaji mazao ya nyuki

MWAKA	MAZAO YA NYUKI		THAMANI YA MAZAO	
	ASALI KGS	NTAKGS	ASALI TSHS	NTA TSHS
2012/13				
2013/14	811,861	35	997,500,000	-
2014/2015				

Jedwali Na. Idadi ya mizinga

MWAKA	MIZINGA YA ASILI/KIENYEJI	MIZINGA YA KISASA	UZAISHAJI KWA MIZINGA	
			KIENYEJI	KISASA
2012/13				
2013/14	230	-	- lita10	- lita 15 hadi 20

NB: Mzinga wa kienyeji huzalisha lita10 za asali kutegemea na ukubwa wa mzinga. Mzinga wa kisasa huzalisha lita 15 hadi 20 kwa msimu.

5.2.1 CHANGAMOTO

- Kutokwepo na duka la pembejeo za ufugaji nyuki wilayani.
- Matumizi ya madawa ya kilimo ambayo yanasababisha vifo vya nyuki.
- Uchomaji moto mapori ambao unaanguza miti muhimu kwa utoaji wa asali vilevile mizinga.
- Ufyekaji wa misitu unaofanywa na wakulima wakati wa kuandaa mashamba mapya ya kilimo

5.2.2 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

- Kushauri wafanya biashara kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa ili kuweza kufungua maduka kwa ajili ya kuuza vifaa vya kuvunia mazao ya nyuki mfano mizinga ya kisasa
- Kushauriana na wataalamu wa idara ya kilimo kuhusu aina ya dawa na muda wa kutumia madawa hayo.
- Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari za uchomaji moto hovy misitu.
- Kuwezesha jamii kuanzisha vikundi vya ufugaji nyuki pamoja na shughuli ambazo ni rafiki wa mazingira kama uoteshaji wa miche ya miti
- Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo.
- Kubuni na kutumia utaratibu sahihi wa kutoa liseni mbalimali za uvunaji wa misitu.
- Kuendeleza kupiga marufuku uvunaji wa mazao ya misitu katika vyanzo vya maji.
- Kuandaa mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi.
- Kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na kuboresha mbinu za ufugaji.
- Kuendeleza kampeni ya elimu ya mazingira kwa jamii.

5.2.3 MATARAJIO:

- Kupungua kwa kiwango cha uharibifu wa mazingira na kuwa na maendeleo endelevu.
- Kukuza uelewa kwa jamii na uwezo wao kushiriki katika hifadhi ya mazingira.
- Jamii kuwa na mipango endelevu ya hifadhi ya mazingira.

6.0 SEKTA YA ARDHI

6.1 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ARDHI.

Halmashauri ya Wilaya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Wataalam wa Sekta ya Ardhi na hatua za kuajiri Wataalam husika zinaendelea. Hali halisi ya Wataalam ilivyo Ki-Wilaya ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini;-

Jedwali Na. Wataalamu wa ardhi

NA	KADA	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
1	Upimaji Ardhi	3	1	2
2	Usimamizi Ardhi	4	1	3
3	Uthamini	1	-	1

4	Mipango miji	1	-	1
5	Uchoraji ramani	2	1	1
	JUMLA	11	3	8

6.2 UPIMAJI VIWANJA

Upimaji viwanja katika makao makuu ya wilaya umeanza na jumla ya viwanja 600 vimepimwa na mchakato wa kuviuza unaendelea.

6.3 MABARAZA YA ARDHI.

Wilaya ya Chemba haina Baraza la Ardhi .Migogoro ya ardhi inashughulikiwa na Baraza la Ardhi la kondoa.Katika Wilaya ya Chemba kuna jumla ya kata **20** ambazo nyingi zimeunda Mabaraza ya Ardhi ya Kata isipokuwa kwenye kata kwamtoro

6.3 UFUMBUZI WA MIGOGORO.

Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imeweza kutambua mipaka yake yote kwa kushirikiana na timu ya taifa ya takwimu (Nbs). Hata hivyo kumekuwa na dalili za kujitokeza kwa migogoro kati ya wafugaji na wakulima kufuatia ongezeko la watu lianalosbabisha wakulima kupanua mashamba na kuvamia maeneo ya malisho.

6.4 CHANGAMOTO:

Katika Wilaya Changamoto zinazoikabili Sekta ya Ardhi ni pamoja na ;-

- tekelezaji wa shughuli za Sekta ya Ardhi ikiwa pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi unakabiliwa na uhaba mkubwa wa Wataalam

wa fani mbali mbali za Sekta za Ardhi katika Halmashauri Uhaba upo katika fani za Upimaji Ardhi, Uthamini, na Usimamizi wa Ardhi.

- Ufinyu wa fedha za kutekeleza shughuli ya kuandaa Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi
- Ukosefu wa vifaa (Vitendea kazi) kama vile, Total Station, Gari n.k.
- Ufinyu wa bajeti unasababiisha Sekta ya Ardhi kutokuwaelimisha wananchi kuhusu Matumizi Bora ya Ardhi, Sheria na Kanuni za Ardhi na Mipango Miji.
- Wananchi kutokuwa na utayari wa kuachia maeneo au mashamba yao yabuniwe viwanja.

7.0 SEKTA YA BARABARA,

Mtandao wa Barabara Wilayani una jumla ya km **928**, Barabara za Wilaya zenye urefu wa km **415** ndizo zinazohudumiwa na mfuko wa barabara.

Jedwali Na.

NA	AINA YA BARABARA	JUMLA	KILOMETA
1	Barabara Kuu		50
2	Barabara za Mkoa		170
3	Barabara za Wilaya		415
4	Barabara za kuunganisha vijiji/kata		293
	JUMLA		928

Katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Halmashauri ya wilaya ilipokea jumla ya Tshs. Milioni 391.7 na kufanya matengenezo ya jumla km 204 kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. .. Matengenezo ya barabara mwaka 2013/14

NA	JINA LA BARABARA	KM	KIASI Tshs. (mil.)
1	Kwamtoro - Swagaswaga	10	20.00
2	Ilasee-Handa	10	10.00
3	Donsee - Maziwa	10	10.00
4	Maziwa - Chase - Makorongo	10	10.00
5	Kelema - Maziwani	10	10.00
6	Songolo - Churuku	10	10.00
7	Jangalo - Chandama	10	10.00
8	Mrijo-Msaada	15	15.00

9	Msaada-Soya	10	10.00
10	Churuku-Kwadelo	15	15.00
11	Chandama - Soya - Mwaikisabe	20	40.00
12	Kwamtoro - Sanzawa - Mpendo	20	40.00
13	Chemba - Mirambo - Goima	18	40.00
14	Chemba - Donsee	20	40.00
15	Tandala - Jangalo - Itolwa	6	60.00
16	Ujenzi wa madaraja/madaraja mfuto(drifti) katika maeneo korofi	1no	28.08
	Gharama za usimamizi na ufuatiliaji	Jml	23.62
	JUMLA KUU	204	391.70

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Halmashauri inatarajia kupokea jumla ya shilingi milioni 620.12 Kwa ajili ya matengenezo ya Jumla ya km 210.8

Jedwali Na... matengenezo ya barabara mwaka 2014/15.

NA	JINA LA BARABARA	KM	KIASI Tshs. (mil.)
1	Jangalo - Chandama	10	10.00
2	Donsee - Maziwa	10	10.00
3	Songolo - Churuku	10	10.00
4	Churuku-Kwadelo	10	10.00
5	Kelema - Maziwani	10	10.00
6	Chemba - Mirambo - Goima	15	15.00
7	Chandama - Soya - Mwaikisabe	15	15.00
8	Kwamtoro - Sanzawa - Mpendo	29	29.03
9	Maziwa - Chase - Makorongo	20	20.00
10	Kwamtoro - Swagaswaga	6	6.00
11	Chemba - Donsee	20	20.00
12	Tandala - Jangalo - Itolwa	15.5	31.01
13	Msaada-Soya	15.5	31.00
14	Chemba - Ombiri - Soya	8.5	85.00
15	Ilasee-Handa	8.5	85.00
16	Mrijo-Msaada	7.81	78.05
17	Ujenzi wa madaraja/madaraja mfuto(drifti) katika maeneo korofi	4no	124.02
	Gharama za usimamizi na ufuatiliaji	Jml	31.01
	JUMLA KUU	210.8	620.12

7.4 MAFANIKIO YA SEKTA YA BARABARA.

Katika Sekta ya Barabara kuna mafanikio katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja kama ifuatavyo:

1. Matengenezo ya kawaida ya barabara yameongezeka kutoka km 82 mwaka 2012/2013 na kufikia km 120 mwaka 2013/2014.
2. Matengenezo ya sehemu korofi yameongezeka kutoka km 48 mwaka 2012/2013 na kufikia km 78 mwaka 2013/2014.
3. Kiwango cha asilimia ya Barabara za Wilaya zinazopitika wakati wote wa mwaka kimeongezeka kutoka 60% mwaka 2012/2013 na kufikia 75% mwaka 2013/2014 kutokana na kuimarisha maeneo korofi.

7.5 CHANGAMOTO TUNAZO KABILIANA NAZO.

- Wakandarasi wengi hawana Utaalam na vitendea kazi, wengi wao hutegemea kukodisha mitambo, hivyo, kusababisha kazi nyingi zisikamilike. katika muda uliopangwa.
- Baadhi ya wananchi wasio waaminifu huchimbua makalvati ya chuma na kukata vyuma vya madaraja na kuharibu barabara kwa malengo yao binafsi.
- Katika maeneo ambayo yanashida ya maji wakati wa kiangazi, wananchi wana tabia ya kuchimba chini ya madaraja na madrifti kwa lengo la kutafuta maji, hivyo kusababisha uharibifu wa miundombinu hiyo.
- Sehemu nyingi wananchi wanamazoea ya Kupitisha mifungo barabarani ambapo mifugi husababisha uhalibifu mkubwa wa barabara.
- Upungufu wa vitendea kazi kama vile gari ya usimamizi wa kazi za barabara, Halmashauri imeandika barua kuomba gari ya usimamizi wa kazi za barabara OWM – TAMISEMI.
- Ufinyu wa bajeti ambayo haitoshelezi mahitaji ya miundombinu ya barabara
- Ukosefu wa wakandarasi wenye uwezo wa kifedha, wataalamu na vifaa

7.6 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.

- Kutenga maeneo maalum kwa ajili ya njia za kupitishia mifugo (stoclo route).

- Kuwaelimisha wananchi juu ya athari za uharibifu wa barabara utokanao na kupitisha mifugo barabarani pamoja na kutochimba miundombinu ya madaraja kwa ajili ya kutafuta maji.
- Kuwashirikisha wananchi katika shughuli za kutunza na kukarabati barabara za vijijini kupitia mpango wa kuendeleza barabara vijijini (V.T.T.P)
- Kuomba Serikali kuajiri watumishi wa kada ya mafundi sanifu na kuongeza vitendea kazi (gari ya usimamizi wa kazi za barabara).

7.6.4 HUDUMA YA mawasiliano

Kampuni zinazotoa huduma ya simu hapa Wilayani ni hizi zifuatazo:

- TTCL
- VODACOM
- TIGO
- ZAIN
- ZANTEL

Uwepo wa Kampuni hizi hapa Wilayani huchangia kukuza uchumi na maendeleo ya jamii kutokana na kurahisisha na kuharakisha shughuli za kiuchumi na kibiashara kama vile taarifa za masoko, huduma za kibenki na mitandao ya kijamii

7.7.5 MAFANIKIO

Sehemu kubwa ya eneo la Wilaya ya Chemba linapokea na kutumia huduma ya mawasiliano ya simu za mkono kwa shughuli za kijamii na kibiashara

7.7.6 CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio niliyo yataja hapo juu bado kuna maeneo ya Wilaya hii ambapo huduma hii haipatikani kabisa , hivyo kufanya mawasiliano ya kijamii na kibiashara kuwa magumu. Hali hii huchangia kukwamisha kasi ya maendeleo ya Wilaya yetu.

7.7.7 MIKAKATI

Tunaendelea kushawishi Makampuni ya Mawasiliano yapanue wigo wa mawasiliano ili kufikia maeneo yote ya Wilaya hii.

7.8 UMEME

Wilaya ya Chemba inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia mradi wa kitaifa wa umeme vijijini REA. Kupitia mradi huu jumla ya vijiji 30 itapatiwa umeme ambao utanufafaisha jumla ya wakazi 235711 watanufaika mara utalokopo kamilika

7.10 UMEME WA NGUVU ZA JUA (SOLAR POWER)

Matumizi ya umeme wa nguvu za jua (Solar energy) yanaendelea

Kuongezeka kwenye majengo ya taasisi za serikali na watu binafsi kama vile Zahanati za vijiji vya kwamtoro, Farkwa na Chemba.

- Matumizi ya watu binafsi vijijini hasa kwenye nyumba binafsi za kuishi na Biashara.
- Matumizi ya Mashine za Kampuni za Simu za TTCL.

7.11 INTANETI

Hudu ma za intaneti zinapatikana hasa katika jengo la muda la makao makuu ya wilaya wakati vijiji ving vya wilaya havina huduma hiyo ya intaneti.

7.12 RADIO

Wakazi wa Wilaya ya Chemba kwa sehemu kubwa wanatatizo la upatikanaji wa masafa ya FM.na hivyo kusababisha wananchi kutopata huduma za radio:-

8.0 SEKTA YA MAJI.

Wilaya haina vyanzo vya kudumu vya maji vilivyo juu ya ardhi ziwa au mito. Hata hivyo Wilaya ina visima virefu 61 na visima vifupi 66. Kiwango cha maji kinachopatikana Wilayani, kwa kiasi cha asilimia 32. Aslimia kubwa ya maji Vijijini ni visima vifupi na virefu, mabwawa na malambo. Miradi iliyosimama na inayotoa huduma ya maji ni kama ifuatavyo:-

JEDWALI NA. 55: Miradi ya maji vijijini

NA	JINA LA MRADI	CHANZO CHA MRADI	HALI YAKE KWA SASA
1	Mondo	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
2	Waida	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
3	Kelema Maziwani	Kisima Kirefu	Unafanya kazi

4	Dalai	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
5	Tandala	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
6	Tandala	Mtiririko	Unafanya kazi
7	Mtakuja	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
8	Mtakuja	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
9	Jangalo	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
10	Mlongia	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
11	Goima	Bwawa	Unafanya kazi
12	Mlongia	Bwawa	Unafanya kazi
13	Jinjo	Bwawa	Unafanya kazi
14	Jinjo	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
14	Churuku	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
15	Churuku	Bwawa	Haufanyi kazi
16	Kinkima	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
17	Paranga	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
18	Sori	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
19	Isini	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
20	Cheku	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
21	Kelema Balai	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
22	Kelema Balai	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
23	Kelema Kuu	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
24	Goima	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
25	Jenjeluse	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
26	Mirambo	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
27	Mirambo	Bwawa	Unafanya kazi
28	Makamaka	Bwawa	Unafanya kazi
29	Songolo	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
28	Madaha	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
29	Hamai	Mtiririko	Mradi unakarabatiwa
30	Chemba	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
31	Kidoka	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
32	Pangalua	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
33	Ombiri	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
34	Ombiri	Mabwawa mawili	Yote yanafanya kazi
35	Kidoka	Bwawa	Unafanya kazi
36	Kidoka	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi

37	Kambi ya Nyasa	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
38	Mrijo Chini	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
39	Nkulari	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
40	Magasa	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
41	Isusumya	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
42	Olboloti	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
43	Olboloti	Mabwawa mawili	Yote yanafanya kazi
44	Mrijo Juu	Bwawa	Unafanya kazi
45	Msaada	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
46	Songambebe	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
47	Msaada	Bwawa	Unafanya kazi
48	Soya	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
49	Mapango	Bwawa	Unafanya kazi
50	Mwailanje	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
51	Wisuzaje	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
52	Mwaikisabe	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
53	Farkwa	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
54	Mombose	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
55	Bugenika	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
56	Gonga	Kisima Kirefu	Mradi unaendelea kujengwa
57	Donsee	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
58	Makorongo	Visima vifupi vitatu	Kimoja ndio ninafanya kazi
60	Babayu	Visima vifupi viwili	Kimoja ndio ninafanya kazi
61	Nkubunko	Visima vifupi viwili	Kimoja ndio ninafanya kazi
62	Maziwa	Visima vifupi viwili	Kimoja ndio ninafanya kazi
63	Makorongo	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
64	Chase	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
65	Chase	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
66	Gwandi	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
67	Rofati	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
68	Humekwa	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
69	Tumbakose	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
70	Hawelo	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
71	Gwandi	Bwawa	Unafanya kazi
72	Kwamtoro	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
73	Poru Banguma	Kisima Kirefu	Unafanya kazi

74	Kurio	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
75	Ndoroboni	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
76	Msera	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
77	Msera	Bwawa	Unafanya kazi
78	Msera	Visima vifupi viwili	Kimoja ndio ninafanya kazi
79	Kurio	Visima vifupi viwili	Kimoja ndio ninafanya kazi
80	Ovada	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
81	Kinyamshindo	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
82	Mengu	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
83	Ovada	Visima vifupi viwili	Vyote havifanyi kazi
84	Kinyamshindo	Visima vifupi viwili	Vyote havifanyi kazi
85	Jogolo	Mtiririko	Unafanyakazi
86	Takwa	Mtiririko	Unafanyakazi
87	Dinae	Visima vifupi vitatu	Kimoja ndio ninafanya kazi
88	Mpendo	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
89	Kubi	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
90	Hamia	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
91	Ilasee	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
92	Lahoda	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
92	Handa	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
93	Magambua	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
94	Wairo	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
95	Manantu	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
96	Magambua	Bwawa	Unafanya kazi
97	Lahoda	Bwawa	Unafanya kazi
98	Manantu	Bwawa	Haufanyi kazi
99	Ilasee	Kisima kifupi kimoja	Kinafanya kazi
100	Kisande	Visima vifupi vitatu	Kimoja kinafanya kazi
101	Sanzawa	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
102	Gumbu	Kisima Kirefu	Unafanya kazi
103	Moto	Kisima Kirefu	Haufanyi kazi
104	Sanzawa	Bwawa	Unafanya kazi
105	Gungi	Visima vifupi vitatu	Kimoja kinafanya kazi
106	Sanzawa	Kisima kifupi kimoja	Kinafanya kazi

8.2 MIFUKO YA MAJI.

Kwa maeneo ya vijijini, sasa kuna jumla ya kamati za maji za vijiji 89 na kamati za watumiaji maji 11 ambazo zinamifuko ya maji yenye jumla ya Tshs 42,101,861/= Jitihada za uundaji wa kamati zingine unaendelea.

Uhamasishaji huo unaenda sambamba na mradi mkubwa wa “National Rural Water Supply and Sanitation Program” (NRWSSP) pamoja na miradi inayotekelezwa Wilayani chini ya wafadhili mbalimbali.

Katika miradi ya visima vyote virefu na vifupi vijijini kwa asilimia kubwa Wilaya imefadhiliwa na wafadhili wafuatao; Benki ya Dunia, Water Aid, BFFS/IFAD, LGCDG, CMSR, World Vision, SABODO Foundation, Caratas, SNV-kridep, etc.

8.3 JUHUDI ZINAZOFANYWA NA WILAYA:-

Juhudi zifuatazo zinafanywa na Halmashauri katika sekta ya maji ili kukabiliana na matatizo yaliyotajwa hapo juu.

- i. Kukarabati mifumo chakavu ya usambazaji maji, na visima vilivyoharibika.
- ii. Kuhamasisha wananchi kuvuna maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba zao kwa wale wenye nyumba za bati au njia ya mabwawa na malambo.
- iii. Uaanzishwaji wa kisheria wa vyombo huru vya utoaji wa huduma ya maji kwa mfano:-
 - Uundaji wa Jumuiya ya Watumiaji Maji mfano – Mwaikisabe, Magasa, Gongu, Kelema Kuu, Jenjeluse, Mtakuja, Olboloti, Mlongia, Pangalua, Wairo na Goima.
 - Uundaaji wa vikundi vya watumiaji maji.
- iv. Ushirikishaji wa Mashirika ya sio ya kiserikali pamoja na makampuni binafsi, umewezesha kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma ya maji vijijini kama inavyoonekana kwenye jedwali.

Jedwal Na. Miradi ya wabia wa maendeleo (development partners)

NA	SHIRIKA/MFADHILI	TARAFU	AINA YA CHANZO	VILIVYO KAMILIKA	HAVIJA KAMILIKA
1	AICC	Kwamtoro	Kisima kirefu	2	2
2	COMPACTION	Goima	Kisima kirefu	1	1
3	ANGLICAN	Goima	Kisima kirefu	1	0
4	SABODO Foundation	Goima, Mondo na Farkwa	Kisima kirefu	8	0

5	Kicheko	Goima	Kisima kirefu	1	1
6	Roman Katoriki	Mondo	Kisima kirefu	1	0
Jumla				14	4

8.4 PROGRAM YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (NRWSSP)

Kwa mradi wa maji wa Kitaifa wa vijiji 22

8.5 PROGRAM NDOGO YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (QUICK - WINS)

Katika utekelezaji wa program hii kwa mwaka 2013/2014 Wilaya inatarajia kupokea jumla ya

shs.1,556,242,527/=

8.7 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI.

- Wananchi kutotunza na kutekeleza vyanzo vya maji vilivyopo.
- Wananchi kutolinda na kutunza mitambo na miundo mbinu iliyopo.
- Uhamasishaji na Elimu zaidi inahitajika kwa wananchi jinsi ya kutunza vyanzo vya maji , mabwawa, visima walivyo navyo ili viwe endelevu.
- Uhamasishaji zaidi unahitajika kwa wananchi kwa ajili ya kuchangia mifuko ya jamii.

8.8.1 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.

- Kuendelea kuibua miradi ya maji na kuchangia utekelezaji wa miradi hiyo.
- Kuendelea kuhamasisha wananchi kuchangia miradi ya maji na kuboresha mifuko ya maji iwe endelevu.
- Kujenga uwezo kwa viongozi wa kamati za maji vijijini ili waweze kuelimisha wananchi wao kuhusu utunzaji wa visima vya maji.
- Kuhamasisha wananchi ujenzi wa nyumba bora za bati kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Kusambaza kwenye kata sheria ndogo za Halmashauri kwa ajili ya uanzishwaji na utunzaji wa vyanzo vya maji.

9.0 AFYA

9.1 MALENGO NA HALI YA UTOAJI HUDUMA ZA AFYA WILAYANI

Lengo ni kutoa huduma za afya kwa wakazi wa wilaya ya Chemba ili kuboresha afya ya watu na mazingira kwa ujumla kwa kutoa tiba na kinga kwa magonjwa mbalimbali kwa wakazi wa wilaya ya Chemba.

9.2 KUPUNGUZA VIFO VYA WATOTO

- Kupunguza vifo vya watoto kutoka 2/1000 hadi 1.8/1000 ifikapo Dec2014.

- Kuongeza vitendea kazi katika vituo vyakutolea huduma, vifaa vyenye thamani ya sh.212,275,400 Vimenunuliwa , vifaa hivi ni magodoro, mashuka, vitanda ,na vifaa vya usafi.
- Kuendesha mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa afya kazini, ili kuboresha huduma kwa wagonjwa
- Kununua madawa yakutosha, Madawa yenye thamani ya Tsh.82, 000,000 yamenunuliwa kwa mwaka huu wa fedha kutoka mfuko wa busket fund.

9.3 KUPUNGUZA VIFO VYA AKINA MAMA KUTOKANA NA UZAZI

- Kupunguza vifo vya akina mama kutoka 82/100000 hadi 42/100000 ifikapo 2015..
- Kuhamasisha jamii ili akina mama wahudhurie kliniki na wajifungulie katika vituo vya kutolea huduma za mama na mtoto.
- Kutoa vyandarua kwa kila mama mjamzito kupitia hati punguzo.
- Kuhakikisha madawa na vifaa tiba vinakuwepo katika vituo vya kutolea huduma kwa kuimarisha zoezi la ukaguzi (drug auditing).
- Kuhakikisha huduma ya uzazi wa mpango inatolewa bure katika vituo vyote
- Kuhakikisha akina baba(wanaume) wanashiriki kikamilifu kumhudumia mama mjamzito, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua
- Kuwahamasisha akina mama wajawazito kutambua Viashiria vya hatari, hivyo kuwahi hospitalini kwa matibabu sahihi.
- Kuhakikisha huduma inayotolewa kwa akina mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano ni bure.
- Watumishi kuendelea kupewa mafunzo ya life serving skills (LS
- Kuanzisha huduma za upasuaji katika vtuo vya Afya. Kwa sasa ukarabati wa chumba cha upasuaji unafanyika katika kituo cha Hamai

9.4 KUDHIBITI UGONJWA WA MALARIA

- Kuendelea kuelimisha jamii juu ya njia sahihi za kujikinga na ugonjwa wa malaria
- Kuendelea kutibu wagonjwa kwa tiba sahihi za malaria kulingana na miongozo ya wizara ya Afya.

- Kuwagawia walengwa vyandarua vyenye viwatilifu vya muda mrefu. Kama kushirikiana na shirika la MEDA kugawa Vyandarua kwa walengwa wote
- Kuendelea kutoa mafunzo ya matibabu kwa uwiano katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya na ngazi ya jamii.
- Kufanya utafiti wa kubaini mazalia ya mbu kwa wilaya ya nzega, ili hatua madhubuti kuchukuliwa

9.5 UZUIAJI WA MAAMBUKIZI VVU KUTOKA KWA MAMA KWENDA KWA MTOTO (PMTCT)

Huduma hii ilianza kutolewa katika wilaya ya Chemba kuanzia julai 2013 kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la **TUNAJALI** ambalo linaendelea na ufadhili mpaka sasa.

Huduma hii imeendelea kutolewa katika vituo takribani 26 kwa wilaya nzima, huduma hii inalenga;

- Kupima VVU kwa akina mama wote wajawazito wanaohudhuria kliniki ya mama na mtoto
- Kupima VVU akina mama wote wanaofika muda wa kujifungua kama hawakupata huduma hii wakati wa kipindi cha ujauzito
- Kuwashirikisha akina baba/wenza nao wapime kwa hiari VVU
- Kutoa dawa aina ya NIVERAPINE, ZIDOVUDINE NA LAMIVUDINE kwa mama na mtoto kuzuia maambukizi,

Kuanzia januari hadi machi akina mama 2536 sawa na 110% walihuzuria kliniki ya mama na mtoto (ANTE NATAL-Clinic). Na huduma ya ushauri na upimaji wa hiari ilitolewa kama ifuatavyo

- Jumla ya akina mama 1234 walipimwa VVU sawa 52%
- Jumla ya akina mama 1227 hawakuwa na maambukizi sawa na 99% kati ya wote waliopimwa
- Jumla ya akinamama 7waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU sawa na asilimia 0.5 %

Huduma hii ya PMTCT ilitolewa pia kwa akinamama waliofika katika vituo vya kutolea huduma kwa lengo la kujifungua.

- Jumla ya akinamama .896. walifika vituoni kujifungua
- Akinamama 1302 hawakupimwa afya zao wakati wa mahudhurio ya kliniki
- Akina mama 1227 walipimwa kliniki na hawakuwa na maambukizi
- Akina mama.7walipimwa kliniki na kukutwa na maambukizi na walipewa dawa aina ya NVP,3TC NA ZDV

- Watoto wapatao 7 walipatiwa dawa aina ya NVPSYRUP
- Akinamama 6 walipimwa afya zao wakiwa katika chumba cha kuzalia
- Akina mama 0 (0%) walikuwa na maabukizi ya VVU
- Watoto 7 waliozaliwa walipewa dawa hiyo ya NVP
- Jumla ya watumishi 17 wamefundishwa njia mpya zindi ya kuzuia VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto (MECR)

9.6 MABORESHO KATIKA SEKTA YA AFYA.

- Kuendelea kuajiri wataalam wenye sifa, Jumla ya watumishi 4 walijiriwa kwa mwaka 2013/14. Aidha wilaya imetengewa jumla ya watumishi 70 wa kada mbalimbali. Hata hivyo bado kuna upungufu wa watumishi 274
- Kuwepo na mpango wa MMAM (Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi), jumla ya kiasi cha Tsh115, 689,050 kwa mwaka 2013/14 zimeidhinishwa katika bajeti na jumla ya Tsh78, 000,000 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji/ukarabati wa zahanati, ujenzi wa nyumba za watumishi, na ununuzi wa vifaa mbalimbali.
- Huduma za akinamama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee kutolewa bure.
- Kuendelea kuhamasisha jamii kuendelea kujiunga na mfuko wa CHF, ili kuboresha huduma kwa mateja
-

9.7 UCHUNGUZI WA MAABARA.

Huduma za uchunguzi wa maabara hufanyika katika Vituo vya Afya 2 na zahanati 33 Aina ya vipimo vinavyochuliwa ni kama ifuatavyo kprima wamama wajawazito HIV/AIDS:

- Blood Smear for malaria parasites, jumla ya sampuli 1034 zilipimwa na sampuli 166 zilikuwa na vimelea vya malaria.
- RPR- kwa ajili ya magonjwa ya zinaa zilikuwa 1372
- Blood sugar -
- HB- wingi wa damu, jumla ya vipimo 370 vilipimwa, wenye upungufu wa damu chini ya 7.0 gm/dl ni 0
- Stool- vipimo vya choo ni 289 na 29 vilikuwa na aina mbalimbali ya minyoo
- AFP- sampuli za makohozi 64 zilipimwa na 3 zilikuwa na vimelea vya TB

- HIV test- wateja 2377 walipimwa VVU
- Sickling Test - sampuli - zilipimwa na- walikuwa na ugonjwa wa sickle cell
- CD 4 count test - jumla ya sampuli 49 zilipimwa
- Haematological test jumla ya sampuli - zilipimwa
- Biochemistry test jumla ya sampuli - zilipimwa
- Grouping and X – matching –

9.9 HUDUMA ZA MAMA NA MTOTO (RCH)

Huduma hizi hutolewa katika vituo 33 vya huduma za afya vilivyopo katika vijiji 33. Aidha huduma kwa kutumia mfumo wa chanjo za mkoba hutolewa katika vijiji 62 visivyo na vituo vya huduma za afya.

Kuna ongezeko la 12 % kwa mwaka 2014 la wajawazito katika hudhulio la kwanza katika vituo vya kutolea huduma.

JEDWALI NA.59. Vifo vya wazazi kuanzia Januari 2013 hadi desemba 2014 na baadhi ya visababishi vya vifo hivyo

Mwaka	Wanawake waliozaa	Watoto waliozaliwa hai	Idadi Ya vifo vya akina mama	Uwiano wa vifo kwa kila 10000 (MMR)	UpunGufu Wa damu	Kifafa Cha mimba	Kutokwa damu b/kuji	Malaria	Kucha Nika Mfuko Wa uzazi	Shinikio la damu	Sababu zingine HIV, L/herbs
2013	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
2014	1220	1217	3	82/1000	7	0	1	0	0	0	-

Januari hadi machi 2014 jumla ya akinamama 3 wamefariki kwa sababu mbalimbali za uzazi kama zinavyoonekana hapo juu; zikiongozwa na upungufu wa damu, kifafa cha mimba , kutokwa na damu

baada ya kujifungua, kuchanika mfuko wa uzazi na shinikizo la damu wakati wa ujauzito. Pia utumiaji wa dawa za kienyeji na ugonjwa wa UKIMWI zimechangia ongezeko la vifo hivi.

JEDWALI NA. 60. Sababu za vifo vya watoto chini ya miaka mitano

Mwaka	Watoto waliozaliwaa Zaliwa hai	Vifo	<5MR	Malaria	Upungufu Wa damu	Pneumonia	Kuharisha	Upungufu wa rishe	Majeraha Ya moto	Poisoning	Mengineyo
2013	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
2014	1220	3		0	0	0	2	0	1	0	0

JEDWALI NA.61 wateja wa uzazi wa mpango

Mwaka	walengwa	Idadi ya wateja wapya	%
2013			
JAN – MARCH 2014	11785	1576	13.3%

Hali ya uzazi wa mpango, kitaifa ni 27% , kiwilaya 13.3% na hili linatokana na imani ya dini inayowapelekea wanaume wengi kutoshiriki vyema katika swala zima la uzazi wa mpango. Tayari asasi mbalimbali kwa kushirikiana na wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zinatoa ufadhili katika swala hili ikiwa ni pamoja na kuelimisha jami na watumishi kazini juu ya swala hili. Pia wanatoa utaalamu na vifaa vya kufanyia kazi katika ngazi zote za kutolea huduma za afya. Asasi hizo ni kama Mariastopes na Engender health

JEDWALI NA.62 hali ya akina mama wajawazito na kujifungu

MWAKA	Taarifa za Kujifungua katika Vituo vya kutolea Tiba				Rufaa	Jumla	Mimba Kuharibika
	Kawaida	Vacuum	Kupasuliwa (C/S)	Njia nyinginezo	-		
2013							
2014	1220	0	0	0		1220	0

HUDUMA YA CHANJO

Idadi ya watoto chini ya mwaka mmoja waliopata chanjo mwaka 2013 ni kama ilivyoonyesha katika jedwali hapo chini

JEDWALI NA. 63A.

	BCG			DPT3	Polio 3	Measles
	%		88%	83.3%	83%	82%
Waliochanjwa			8317	7848	7821	7746
Walengwa			2366	9428	9428	9428

